# TNMC Habari

Toleo NO. 008

Jarida la Mwezi Mei, 2024

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari


## TAMISEMI, AFYA, UTUMISHI WASISITIZWA KUMALIZA CHANGAMOTO ZA WAUGUZI NCHINI

Uk 01



## TNMC YAWASIMAMISHA WAUGUZI NA WAKUNGA 09 KUTOA HUDUMA




- *Nane wapewa ONYO .*
- *Adhabu zote zatolewa kwa mujibu wa Sheria*

Uk 06

## TRILION 1.3 KUTEKELEZA VIPAUMBELE 10 VYA WIZARA YA AFYA

Uk 02

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI


**MWENYEKITI**

Bi. Agnes Mtawa

**MHARIRI**

Mwakapiso Ndimmyake

**WARATIBU**

Irene Chilewa
Rose Mhando

**MSANIFU JARIDA**

Ezekiel Nyalusi



P.O BOX1736 DODOMA
TEL.022-212133975 Fax.022-2133975 Mobile:0786785947

# TAMISEMI, AFYA, UTUMISHI WASISITIZWA KUMALIZA CHANGAMOTO ZA WAUGUZI




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko katika maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani - Tanga*

***Na Mwandishi Wetu - Tanga***

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Afya, na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zimesisitizwa kufanyia kazi changamoto zinazowakabili wauguzi nchini ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Agizo hilo limetolewa leo Mei 12, 2024 Jijini Tanga na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, wakati akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani.

Dkt. Biteko amesema, wauguzi ni asilimia 60 ya watumishi katika sekta ya Afya na mchango wa huduma zao katika sekta hiyo ni asilimia 80 na hivyo ni muhimu wanataaluma kuthaminiwa na kuaminiwa pamoja na kupewa dhamana ya madaraka kama ilivyo kwa taaluma nyingine.

***"Uuguzi ni taaluma muhimu hatuwezi kumfanya kuwa daraja la pili katika utendaji kazi ikiwemo nafasi za uongozi, Wizara ya Afya liangalieni hili ndani ya mwaka huu wa fedha unaoisha Juni, 30 jambo hili liwe limefanyiwa kazi"***, amesema Dkt. Biteko.

Amesisitiza kuwa changamoto za wauguzi zimewasilishwa kwa viongozi wakuu wa kitaifa akiwemo Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Isdor Mpango, ambao kwa nyakati tofauti wametoa maelekezo ya kufuatiliwa na kupatiwa suluhu.

***"Viongozi wametoa maelekezo juu ya suala hili, mimi siwezi kutoa maelekezo tofauti bali kufuatilia utekelezaji wa maelekezo hayo na bahati nzuri nasimamia uratibu wa shughuli za Serikali na hili ni mojawapo",*** alisisitiza.

***"Kama inawezekana wambieni inawezekana na kama haiwezekani wambieni haiwezekani ili suala hilo limalizike"*** ameongeza Dkt. Biteko.

Amefafanua kuwa tayari amewasiliana na Utumishi ambao wako tayari kulifanyia kazi suala la wauguzi kujiendeleza kitaaluma kwa vile wanakwenda kusoma si kwa faida yao binafsi bali wananchi wanaokwenda kupata huduma.

Aidha, Dkt. Biteko, amebainisha kuwa Serikali inafanyakazi kubwa ya kuimarisha miundombinu na imeendelea kuweka kipaumbele katika kuimarisha sekta ya Afya huku akitolea mfano ujenzi wa nyumba za watumishi wa sekta hiyo ambapo kutoka mwaka 2021 hadi 2023 jumla ya nyumba 308 zimejengwa, vituo vya Afya vya upasuaji kutoka 340 hadi 523 kwa lengo la kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora na hivyo ni muhimu kuangalia uwekezaji huo katika eneo la rasilimali watu.

Amesema pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo, wauguzi waendelee kuhimizana katika kutimiza wajibu wao huku akiwaasa Watanzania kuwatia moyo wauguzi wakati wakiwa wanatekeleza majukumu yao.



Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Afya, Dkt. Godwin Mollel kwa niaba ya Waziri wa Afya, Mhe. Ummy Mwalimu, amewahimiza wauguzi kuendelea kufanya kazi kwa kushirikiana ili kuboresha huduma za Afya nchini.

Naye, Rais wa Chama cha Wauguzi Tanzania, Alexander Baluhya, amemueleza Naibu Waziri Mkuu kuwa, wauguzi hao wakiwa mkoani Tanga wamefanya shughuli mbalimbali ikiwemo kuchangia damu, kuhamasisha wananchi kufanya vipimo kwa hiari ikiwemo VVU, tezi dume, shinikizo la damu na magonjwa yasiyoambukiza.

Katika hatua nyingine, wauguzi hao wamekula kiapo cha uaminifu ikiwa ni kujikumbusha Sheria, kanuni na taratibu za kutoa huduma bora kwa wananchi.

Maadhimisho hayo ya siku ya Wauguzi Duniani yamehudhuriwa na wauguzi kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na yameongozwa na kaulimbiu inayosema ***"Wauguzi; sauti inayoongoza, wekeza katika uuguzi, heshimu haki linda Afya"***

# TRILION 1.3 KUTEKEZELEZA VIPAUMBELE 10 WIZARA YA AFYA



*Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, wakati akiwasilisha Hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2024/25 Bungeni Jijini Dodoma*

## BUNGE LAPITISHA TRILIONI 1.3 BAJETI MPYA 2024/25

*Na Mwandishi Wetu*

Wizara ya Afya imepanga kutekeleza vipaumbele 10 kwa kutumia afua 86 zinazokadiriwa kutumia kiasi cha shilingi Trilioni 1.3 kwa mwaka ujao wa Fedha 2024/25 itakayohusisha mapato, matumizi ya kawaida na miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mwaka huo.

Hayo yamebainishwa, Mei 13.2024 na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu wakati akiwasilisha Hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2024/25 Bungeni Jijini Dodoma kupitia Bunge la 12, Mkutano wa 15, Kikao cha 24 ambapo ametaja vipaumbele hivyo kuwa ni pamoja na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ambapo katika eneo hilo kiasi cha shilingi 117, 611,588,304 kimetengwa

Vipaumbele vingine ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa ubora wa huduma za Afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za Afya katika ngazi zote ambapo jumla ya shilingi 219,010,767,716 zimetengwa ili kutekeleza eneo hilo, sambamba na hilo liko suala la kuimarisha huduma za Afya za uzazi, Mama na Mtoto ambapo kwenye eneo hilo kiasi kilichotengwa ni shilingi 17,189,250,000

Waziri Ummy, ametaja vipaumbele vingine kuwa ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa wataalam katika sekta ya Afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi ambapo kwenye eneo hilo kiasi kilichotengwa ni shilingi 74,000,000,000, hiyo ikienda sambamba na kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini ambapo kiasi kilichotengwa kwenye eneo hilo ni shilingi 89,858,609,000.

Aidha, katika vipaumbele hivyo lipo suala la kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala ambapo kiasi cha shilingi 1,500,000,000 kimetengwa, kuimarisha udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa ya mlipuko na huduma za Afya za dharura ambapo kwenye eneo hilo Wizara imetenga kiasi cha shilingi 84,864,241,569, na kuimarisha huduma za Afya ya akili ambapo kiasi kilichotengwa kwenye eneo hilo ni shilingi 5,618,528,988.

Pia, Wizara ya Afya imegusia suala la kuimarisha huduma za utengamao na tiba shufaa hususani kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu ambapo kiasi cha shilingi 3,700,000,000 kimetengwa kwenye eneo hilo.

Vipaumbele vingine vilivyowekwa na Wizara ya Afya kwa mwaka ujao wa Fedha ni pamoja na kusimamia tafsiri na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za Afya ambapo kiasi kilichotengwa ni shilingi 3,508,968,000.

# WANAFUNZI WA TANGA COHAS WAPATA MAFUNZO USAJILI WA AWALI *(STUDENT INDEXING)*

***Na Ezekiel Nyalusi***

Wanafunzi wa Chuo cha Afya na Sayansi shirikishi Tanga (COHAS) wamepata mafunzo juu ya umuhimu wa usajili wa awali (Student Indexing) katika mfumo wa Baraza la Uuguzi na Ukunga (TNMCIS) ikiwa ni Mkakati wa kujenga uelewa juu ya matumizi ya mfumo huo ili kupunguza makosa yanayojitokeza wakati wa kujisajili.

Akifafanua juu ya umuhimu wa usajili wa awali, Mkuu wa kitengo cha Mitihani kutoka kurugenzi ya Mafunzo na Maendeleo ya Taaluma Sethbert Haramba, amefafanua kuhusu umuhimu wa kujisali kwa hatua ya awali (student Indexing) pamoja na uhakiki wa sifa za kila wanachuo mara tu anapojiunga na Chuo chochote cha kada ya Afya hapa nchini.

*"Ni muhimu kufanya zoezi la (Student indexing) mapema na hii inatakiwa kufanyika mara tu unapojiunga na Chuo ambacho umedahiliwa kabla hujaanza masomo ili kuepuka kupoteza gharama kwa kutoa Fedha ya ada wakati ufaulu wako katika ngazi ya Sekondari onaonesha huna sifa za kusoma taaluma ya Uuguzi na Ukunga"* alisema Haramba

Haramba, amezitaja faida nyingine za usajili wa awali kuwa, husaidia kufuatilia maendeleo ya ujifunzaji na ufundishaji katika vyuo wanavyosoma ili kupata wataalamu wenye ubora unaotarajiwa na akasisitiza kuwa usajili huu unafanyika kwa mujibu wa kanuni ya Baraza kifungu 14-(1)(2) ya mwaka 2010.

Kwa upandewake mwanasheria wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania George Shilla, amewasisitiza wanafunzi hao kupata muda wa kupitia Sheria, kanuni na miongozo ya Baraza iliyopo kwenye TOVUTI ya Baraza *www.tnmc.go.tz* ili waweze kulifahamu Baraza pamoja na mambo mengine yanayowahusu,

*"Ni vizuri mkaisoma Sheria hii ya mwaka 2010 itawasaidika kujua mipaka na wajibu wenu mkiwa kama wauguzi na wakunga watarajiwa, Sheria imebeba mambo mengi yanayokuhusu wewe"* alisema Mwanasheria Shilla.

Wakitoa mtazamo wao mara baada ya kupata mafunzo hayo wanafunzi wamelipongeza Baraza kwa kutoa elimu na maelekezo, na kusema wamepata mwanga wa kulijua Baraza na majukumu yake sambamba na kufahamu mipaka yao pamoja na majukumu yao kama wanafunzi.

Naye Mkufunzi aneshughulikia taaluma chuoni hapo Bwana Avin Njoki, amesema, umuhimu wa mafunzo hayo yatakuwa na tija katika tasnia ya Afya kwani wanafunzi wanakwenda kuyaishi mafunzo hayo wakiwa shuleni, kazini na hadi wanapokwenda kustaafu.




*Wanafunzi wa kada ya Uuguzi na Ukunga baada ya kupata Mafunzo ya Usajili wa awali katika Chuo cha Sayansi shirikishi Mkoani Tanga.*

# MSAJILI TNMC: TUTOE MAONI YA SHERIA YA UUGUZI NA UKUNGA







*Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa, akiongea na wauguzi na wakunga mkoani Tanga juu ya uboreshwaji wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania.*

## *Na Ezekiel Nyalusi*

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa amewataka wauguzi na wakunga nchini kutoa maoni juu ya uboreshwaji wa sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Ameyasema hayo katika Mkutano wa Mwaka wa chama cha wauguzi Tanzania (TANNA) katika kuelekea siku ya wauguzi Duniani uliofanyika Mkoani Tanga.

*"Suala la kutoa maoni ni la kila Muuguzi na Mkunga hivyo ni vyema kila mtu akashiriki kwa kutoa mawazo yake wapi tuiboreshe Sheria yetu hii na ninaomba tutumie email ya Baraza Info@tnmc.go.tz au ya mwanasheria wetu wa Baraza george.shilla@tnmc.go.tz maoni tutayapokea na kuyafanyia kazi"* alisema Bi. Mtawa

Naye Mwanasheria wa Baraza George Shilla, amesema mpango wa kukusanya maoni ya uboreshaji wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ni ya kitaifa na tayari mikoa ya Njombe, Lindi, Mtwara na Mbeya wamewasilisha maoni yao hivyo ni vyema kutumia wasaa huu kuwasilisha mawazo yenu kuhusu uboreshaji wa Sheria hili

Hata hivyo, baadhi ya wauguzi na wakunga nchini tayari wameshaanza kutuma maoni yao kwenye email ya Baraza kwa lengo la uboreshaji wa sheria hiyo.

Sheria ya Uuguzi na Ukunga Tanzania ilitungwana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010 kwa lengo la kusimamia taaluma ya Uguzi na Ukunga Tanzania ili kuhakikisha jamii inapata huduma zilizo bora na salama.

# UFAHAMU UGONJWA WA FISTULA NA MADHARA YAKE KWA JAMII

## MAKALA MAALUMU

*Na Ndimmyake Mwakapiso*

**NASURI MAARUFU KWA JINA LA FISTULA** ni shimo ambalo hutokea katikati ya kibofu cha mkojo na uke au katikati ya njia ya haja kubwa na uke wa mwanamke ambaye amejifungua kwa shida, Shimo hili hutokea pale ambapo kichwa cha Mtoto ni kikubwa kuliko njia ya uzazi.

Fistula, inasababishwa na uchungu pingamizi ambapo Mama mjamzito husukuma Mtoto kwa muda mrefu wakati wa kujifungua bila usaidizi au matibabu yoyote jambo ambalo husababisha Mama kuchanika (Kutoboka) katika njia ya uzazi na kusababisha tundu ambalo pia husababisha uvujaji wa kinyesi na mkojo bila kujizuia,tundu hili hujulikana kama Fistula.

Aidha, sababu kubwa za kutokea kwa ugonjwa huu ni kama vile kujifungua mapema kabla ya kufikisha umri wa kuanzia miaka 18 yaani mimba za utotoni, ambayo kimekuwa chanzo kikubwa cha kutokea kwa ugonjwa wa fistula kwa kuwa njia ya mzazi na vyonga zake inakuwa haijapevuka vya kutosha kumudu tendo la kujifungua.



Wataalamu wa Afya wanaendelea kubainisha sababu nyingine za fistula kuwa mara nyingi, hutokea kwa wanawake wanaojifungulia majumbani baada ya kukosa matibabu hivyo inashauri kuwa ni vema na kwa wajawazito kujifungulia katika kituo cha matibabu ili waweze kufuatiliwa na kupata huduma za matibabu haraka na kwa wakati.

Vile vile wanawake ambao tundu la kizazi chao ni dogo sana au wale ambao wamekeketwa wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata maradhi hayo.




### NI ZIPI DALILI ZA FISTULA?

Ukiona dalili zifuatazo ni ishara kuwa ukabiliwa na tatizo la ugonjwa wa fistula; Kama unahisi kutokwa na mkojo bila kujizuia, harufu mbaya, maumivu makali sahemu za uzazi, unashauriwa kuwahi hospitali au kituo cha Afya kilicho karibu ili upate ushauri na matibabu zaidi. Matibabu ya fistula ni bure katika hospitali zote nchini.

### MADHARA YA FISTULA

MADHARA KIMWILI

1.Kutokwa na haja ndogo na kubwa au vyote kwa pamoja bila kujizuia

2. Kuungua au kupata vidonda sehemu za siri

**MADHARA KISAIKOLOJIA**

3. Huleta hali ya kutojiamini inayoweza kupelekea sonona

**MADHARA KIJAMII**

4. Unyanyapaa, kutelekezwa na watu wa karibu na kushindwa kushiriki shughuli za kijamii.

5.Familia nyingi huvunjika kutokana na unyanyapaa, Matatizo mengine ya kiafya yanayotokana na maradhi hayo ni ukosefu wa maji ya kutosha mwilini na utapiamlo.

### MADHARA KIUCHUMI

Kushindwa kufanya shughuli za kujiingizia kipato

### NINI KIFANYIKE KUZUIA?

Ni rahisi kuzuia ugonjwa huu iwapo Mama atapata usaidizi wa haraka wa kimatibabu.

Muhimu wasichana na wanawake wapate ushauri jinsi wanavyoweza kuepukana na mimba za mapema kwani miili yao huwa haijakomaa ipasavyo ili kukabiliana na ujauzito na uchungu wa kujifungua.

Wasichana wanaoshika mimba wakiwa wangali wachanga wamo katika hatari kubwa ya kuathirika na maradhi haya zaidi ya wale ambao wamefikia miaka 20.

### MATIBABU YA FISTULA.

Fistula inatibika. Takribani asilimia 90 ya visa vya fistula vinaweza kutibiwa kupitia upasuaji ambao huziba tundu hilo.

Wakati mwanamke anazidi kupona ni vyema azidi kufanya mazoezi ya kuimarisha misuli ya uke ili kurejesha hali yake ya kawaida.

### HITIMISHO;

Kulingana na utafiti wa shirika la Afya Duniani WHO na ripoti iliochapishwa na The Citizen, takribani wanawake milioni mbili wameathirika na fistula.

Idadi kubwa ya wagonjwa hao wanaishi katika Bara la Afrika huku nusu yao ni kutoka nchini Nigeria, hata hivyo ripoti hiyo inabainisha kuwa takwimu hiyo sio kamili au idadi halisi kwani wengi wao wanahofia kujitokeza kwa kuogopa unyanyapaa.

# TNMC YAWASIMAMISHA WAUGUZI NA WAKUNGA 09 KUTOA HUDUMA




*Mwenyekiti wa Bataza Prof. Lilian Mselle(katikati), akizungumza na vyombo vya habari Jijini Dodoma baada ya maamuzi ya kikao cha Baraza dhidi ya tuhuma zilizokuwa zikiwakabili wauguzi na wakunga nchini.*

## Na Ndimmyake Mwakapiso

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) ni mamlaka ya kisheria inayosimami taaluma na wanataaluma wa kada ya uuguzi na ukunga Tanzania Bara chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake, limewasimamisha kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga, wauguzi na wakunga 09 kwa vipindi tofauti tofauti, huku wengine 08 wakipewa ONYO.

Akizungumza na wanahabari Jijini Dodoma, Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Prof. Lilian Mselle, amebainisha kuwa, adhabu hizo zimetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga na kanuni zake ya mwaka 2010, baada ya Baraza kuketi kwa siku mbili kusikiliza tuhuma zilizokuwa zikiwakabili wauguzi na wakunga kutoka mikoa mitano nchini ambayo ni Tanga, Geita, Mara, Shinyanga pamoja na Mkoa wa Morogoro kama ifuatavyo;

Wauguzi na wakunga wawili 02 kutoka kituo cha Afya Mikanjuni Jijini Tanga, wamesimamishwa kutoa huduma kwa kipindi cha miaka 02 na mmoja miezi sita 01, kwa kosa la kushindwa kudumisha viwango vya taaluma ya Uuguzi na Ukunga.

Aidha, Wauguzi 04 wa kituo cha Afya kibaoni Mjini Ifakara na wauguzi 02 kutoka hospitali ya Wilaya ya Mkuranga wote wamepewa adhabu ya ONYO kwa kushindwa kudumisha viwango vya taaluma na maadili ya Uuguzi na Ukunga.

Wauguzi wengine 04 wa hospitali ya Mji Geita, mmoja amesimamishwa kutoa huduma kwa kipidi cha mwaka 01, wawili miezi 06 na mmoja ONYO kwa kosa la kushindwa kudumisha viwango vya taaluma na maadili.

Kituo cha Afya Nyakumbu Kahama,wauguzi na wakunga wawili wamesimamishwa kutoa huduma kwa kipindi cha miezi 06 na wawili wamepewa ONYO kwa kushindwa kudumisha viwango vya taaluma na maadili.

Aidha, Prof. Mselle, amefafanua kuwa adhabu zote zimetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010 kifungu cha 28(3) kwa kuzingatia uzito wa kosa na ushiriki wa mtuhumiwa katika kosa husika.

Katika hatua nyingine Prof. Mselle, amewataka wauguzi na wakunga kuacha tabia ya kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga pasipokuwa na leseni au kwa leseni zilizokwisha muda wake ,na kuwaasa waajiri wote nchini wasikubali kufanya kazi na wauguzi na wakunga wasiyokuwa na leseni na ambao hawajahuisha leseni zao.

Prof. Mselle ameongeza kuwa Sheria ya Uuguzi na Ukunga iliyotungwa na Bunge mwaka 2010, imebainisha adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita au faini isiyozidi Shilingi Milioni moja 1,000,000 au vyote kwa pamoja na hii ni kwa muuguzi husika au mwajiri yeyote anayemwajiri au kuendelea kufanya kazi na muuguzi asiye na leseni au anatumia leseni iliyokwisha muda wake.



# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga limepokea kwa masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele za haki Mwezi Mei Mwaka 2024, baada ya kumaliza kazi yao hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao mahali pema Peponi AMINA.



**JINA: MARY W. JOSEPH**
**KITUO :** St.Agnes
**WILAYA :** Mkalama
**MKOA :**Singida



**JINA: JOFREY J. PAMBA**
**KITUO :** Chemba Health Center
**WILAYA :** Chemaba
**MKOA :** Dodoma

# MATANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA — BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

## USAJILI WA AWALI (STUDENTS INDEXING)

Ofisi ya Msajili Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania linawatangazia Wanafunzi wote wa kada za Uuguzi na Ukunga nchini ambao hawajakamilisha usajili wa awali **(Student indexing)** kuwa, Baraza limeongeza muda wa usajili, ambapo dirisha la usajili limefunguliwa tena kuanzia tarehe **01.06.2024** hivyo, kila mwanafunzi atatakiwa kukamilisha usajili kabla au ifikapo tarehe **30.06.2024** kupitia Mfumo wa Baraza ***https://www.tnmcis.tnmc.go.tz***

Usajili huu ni muhimu na unafanyika kwa mujibu wa kanuni ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 kifungu cha 14-(1) (2).

Nyaraka muhimu wakati wa kutekeleza zoezi hili ni pamoja na;
1. Pasipoti picha 45 X 35mm ***background bluu***
2. Nakala halisi ya cheti cha kuzaliwa
3. Nakala halisi ya cheti cha kidato cha nne (wote) na siyo hati ya matokeo
4. Nakala halisi ya cheti cha kidato cha sita (kwa wanafunzi wa ngazi ya Shahada - ***pre-service***)
5. Leseni hai kwa wanaojiendeleza.

Tunawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na;
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano
TNMC

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA — BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

## MAOMBI YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI AGOSTI, 2024

Dirisha la maombi ya Mtihani litafunguliwa rasmi kuanzia tarehe **01.07.2024** hadi tarehe **14.08.2024.**

Maombi yatafanyika kwa njia ya mtandao kwa kutumia mfumo wa Baraza ***(https//tnmcis.tnmc.go.tz)*** Kila mwombaji atatakiwa kujisajili na kulipia kiasi cha **Shilingi 150,000/=** kwa wale wanaoomba kufanya mtihani huu kwa mara ya kwanza na **Shilingi 75,000/=** kwa wanaorudia.

Waombaji wote mnajulishwa kuzingatia masharti yafuatayo;
**1.** Awe na **Indexing number**
**2.** Awe na picha yenye viwango **(Passport Size 45x35mm)** Blue Background)
**3.** Majina sahihi yanayoendana na **cheti** cha kuhitimu elimu ya kidato cha Nne
**4.** Awe na kadi/ **namba ya NIDA.**
Mtihani utafanyika katika vituo vitakavyopangwa katika mikoa ya **Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Dodoma.**

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:0737-96-26-91**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA